Mpendwa Wetu Mtenda Kazi Pamoja Nasi

na

Terry Warford

Mpendwa Wetu Mtenda Kazi Pamoja Nasi

na

Terry Warford

Novemba 5, 2011

Mpendwa Wetu Mtenda Kazi Pamoja Nasi

Filemoni ni moja kati ya vitabu vifupi na vilivyoboreshwa katika Agano Jipya. Kuna sura moja tu ya mistari 25. Vile vile kuna kuna maana nyingi katika kitabu hiki.

Kati ya vitu vingi tunavyoweza kujifunza, kuna mitazamo mitatu ya ibada ya Mkristo katika hiki kitabu kifupi cha Filemoni. Vitu hivi vitatu vya ushirika ni kuwa watenda kazi- wenza, askari- wenza, na wafungwa-wenza wa Yesu Kristo. Cha kwanza kinafunuliwa katika msitari wa kwanza. "*Paulo mfungwa wa Yesu Kristo, na Timotheo aliye ndugu yetu, kwa Filemoni mpendwa wetu, mtenda kazi pamoja nasi.*"

Fikiria jinsi inavyoweza kuwa vizuri kama ungeweza kupokea barua kutoka kwa Mtume Paulo akikutaja kwamba "*mpendwa*" na "*mtenda kazi pamoja nasi".* Hata hivyo Paulo alikuwa anamuweka Filemoni katika hali ya mshituko katika kujaribu kumpatanisha na Onesimo, salamu kama hiyo kimsingi unaweza kujisikia vizuri.

Lakini ilikuwa ni zaidi ya salamu. Paulo alikuwa anatambua kazi nzuri ambayo Filemoni alifanya kama Mkristo. Soma mistari ya 4-7, "*Namshukuru Mungu wangu sikuzote, nikikukumbuka katika maombi yangu; nikisikia habari za upendo wako na imani uliyo nayo kwa Bwana Yesu na kwa watakatifu wote; ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu katika Kristo. Maana nalikuwa na furaha nyingi na faraja kwa sababu ya upendo wako, kwa kuwa mioyo ya watakatifu imeburudishwa nawe, ndugu yangu.*"

Tukifanya kazi pamoja majina yetu yanaandikwa Mbinguni, tukisoma katika Wafil. 4:3, "*Naam, nataka na wewe pia mjoli wa kweli uwasaidie wanawake hao; kwa maana waliishindania injili pamoja nami, na Klementi naye, na wale wengine waliotenda kazi pamoja nami, ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima.*"

Tunapowasaidia ndugu zetu na dada zetu katika Kristo, tunafanya mema kwa Yesu. Math. 25:40, "*Na Mfalme atajibu, akiwaambia Amin, nawaambia kadiri mlivyomtendea mmoja wapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.*"

Sisi ni watenda kazi wenza sit u kwa kila mmoja, bali na Mungu pia. 1 Wakor. 3:9, "*Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jingo la Mungu.*"

Wengine walitambuliwa kama watenda kazi wenza vilevile, katika Filemoni msitari wa 24, "*Na Marko, na Aristarko, na Dema, na Luka, watenda kazi pamoja nami.*"

Dhumuni la pili la ushirika tunaipata katika msitari wa pili wa Filemoni, "*Na kwa Afya ndugu yetu, na kwa Arkipo askari mwenzetu, na kwa kanisa lililo katika nyumba yako.*"

Maisha ya Mkristo mar azote ni vita vigumu. Ulimwengu unatutupia mengi kwetu, na kwa watoto wetu. 2 Tim. 2:3-4, "*Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.*"

Lakini hatupaswi kupigana vita hivi pekee yetu. Tuna kila mmoja kama askari wenzetu. 1 Petr. 5:8-9, "*Mwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba aungurumaye huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo mkiwa thabiti katika imani mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zetu walioko duniani.*" Na tuna Mungu upande wetu, na anahakikisha ushindi wetu, 1 Wakor. 15:57, "*Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Mungu anatupa silaha kujilinda sisi wenyewe. Waef. 6: 14-18, "*Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu tupatao kwa Injili ya amani, zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.*" Kumbuka kwamba hakuna uongo kwa ajili ya neno. Tumia neno la Mungu kwa hali, kila siku. Na ukumbuke kwamba kukesha na kuomba ni vitu muhimu katika silaha zetu.

Tunasoma dhumuni linguine la tatu inafunuliwa katika kitabu cha Filemoni katika msitari wa 23, "*Epafra aliyefungwa pamoja namei katika Kristo Yesu, akusalimu.*"

Paulo alifanyika mfungwa kwa kuhubiri jina la Yesu, kama tunavyoona katika Matendo 28:16-17, "*Tulipoingia Rumi Paulo alipewa ruhusa kukaa kwake mwenyewe pamoja na askari aliyemlinda. Ikawa baada ya siku tatu akawaita wakuu wa Wayahudi wakutane, hatawalipokutanika akwaambia, ndugu zangu ningawa sikufanya neno kinyume cha watu wetu wala neno lililopingamana na desturi za baba zetu, nalitiwa katika mikono ya Warumi, hali nimefungwa, tokea Yerusalemu.*"

Wengine katika siku hizi walifungwa kwa imani pia. Kwa nyongeza kwa Epafra katika kitabu cha Filemoni, tunasoma katika Warumi 16: 7, "*Nisalimieni Andronikо na Yunia, jamaa zangu waliofungwa pamoja nami, ambo ni maarufu miongoni mwa mitume; nao walikuwa katika Kristo kabla yangu.*" Na katika Wakol. 4:10 tunaona mfano mwingine, "*Aristarko, aliyefungwa pamoja nami, awasalimu; na Marko, mjomba*

wake Barnaba, ambaye mmepokea maagizo kwa habari yake; akifika kwenu mkaribisheni."

Hatakama alishikiliwa kama mfungwa, aliendeleza kazi yake ya kumhubiri Yesu Kristo kwa ye yote na wote ambao wangelisikia. Na wajibu wake kwa kazi yake iliwavuvia wengine, Wafil. 1:12-14, "*Lakini ndugu zangu nataka mjue ya kuwa mambo yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuieneza Injili; hata vifungo vyangu vimekuwa dhahiri katika Kristo, miongoni mwa askari na kwa wengine wote pia. Na wengine wa hao ndugu walio katika Bwana, hali wakapata kuthibitika kwa ajili ya kufungwa kwangu, wamezidi sana kuthubutu kunena neno la Mungu pasipo hofu.*"

Na sisi, kama Paulo na wengine wa siku hizo, tuendelee kusimama imara na kuhubiri Yesu katika uso wa ulimwengu huu wenye uovu. 2 Tim. 1:8, "*Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya Injili,kwa kadiri ya nguvu ya Mungu.*"

Kuna mengine mengi tunayoweza kujifunza kutoka katika kitabu cha Filemoni. Lakini tulitaka kulenga katika kipengele hiki katika mambo matatu ya ushirika. Ushirika ni wakati mzuri wote tunaokuwa nao pamoja; lakini pia inafanya kazi pamoja, kupigana pamoja dhidi ya Shetani, na mar azote kuteseka pamoja. Tunaitajika kuwepo pale kwa ajili yaw engine kwa wakati mzuri na mbaya, tunaposoma katika Waru. 12:15, "*Furahini pamoja nao wafurahio; lieni pamoja nao waliao.*"

Usikatae kitabu kidogo cha Biblia. Hebu na tujifunze katika yote, na kuyatumia katika maisha yetu, ili kwamba tuweze kutambuliwa na Mungu siku ya hukumu kama wapendwa watenda kazi pamoja.

Katika upendo wa Wakristo,

Ndug. Terry Warford